# Mzozo wa Majumbani na Kifamilia

## Nchini Australia, Mzozo wa Majumbani na kifamilia haukubaliki.

Mzozo wa Majumbani na kifamilia ni uhalifu wa kinyume cha sheria.

Mtu anayetenda uhalifu huu anaweza kwenda jela, awe mwanamume au mwanamke.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, wapigie simu polisi, nambari ya simu **000.**
Polisi nchini Australia ni wazuri na wanaweza kuaminiwa.

Kwa maelezo na ushauri wa faragha bila malipo, piga simu1800 RESPECT nambari ya simu
**1800 737 732.**

Kama unahitaji mkalimani bila malipo piga simu **131 450.**

## Australian Government (Serikali ya Australia) haivumilii Mzozo wa Majumbani na familia chini ya hali yoyote ile.

Mzozo wa Majumbani na familia ni pamoja na tabia au vitisho ambavyo vina lengo la kudhibiti mpenzi wa kiume au kike na kusababisha hofu au kutishia usalama wao. Mzozo wa Kinyumbani na familia unajumuisha:

- kupiga;
- ugomvi.
- kunyima fedha muhimu kwa mpenzi au familia;
- kumtenga mpenzi kutoka kwa marafiki na familia;
- matusi au kukosoa mpenzi mara kwa mara; na
- kutishia watoto au mifugo.

## Wanawake wana haki sawa na wanaume.

Sheria za Australia zinachukulia wanawake na wanaume sawa.

Kila mtu ana haki ya kuishi huru dhidi ya Mzozo, katika uhusiano na jamii yenye furaha.

Wanawake hawatakiwi kukubali kuchukuliwa vibaya au kuumizwa.

## Kuna huduma za kijamii nchini Australia ambazo zinaweza kukusaidia.

**1800 RESPECT** ni Australia's National Sexual Assault, Family and Domestic Violence Counselling service (Huduma ya Ushauri wa Mzozo wa Kijinsia, Uhasama wa Kifamilia na Kinyumbani kutoka kwa Taifa la Australia) . Hutoa simu bila malipo na ushari na maelezo mtandaoni. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za usaidizi katika eneo lako

Piga simu **1800 737 732** au nenda kwenye tovuti ya 1800 RESPECT **www.1800RESPECT.org.au**.

## Je unahitaji mkalimani?

Pigia simu **Translating and Interpreting Service (Huduma ya Utafsiri na Ukalimani)** (TIS) bila malipo, nambari ya simu **131 450**. TIS inaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma nyingine. TIS haitoi ushauri.